



# TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

## DHIBITI CHUMVI SHAMBANI KUZALISHA MPUNGA MWINGI

### VYANZO VYA CHUMVI KWENYE UDONGO

- Miamba ya asili yenye chumvi
- Kumwagilia maji yenye chumvi
- Miundombinu mibovu ya umwagiliaji
- Upungufu wa maji  
matumizi mabaya ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo
- Matumizi ya maji toka mashamba mengine, viwandani au makazi

### AINA TATU KUU ZA UDONGO WENYE CHUMVI

- Udongo wa Chumvi (Salaini)
- Udongo wa Magadi (Sodiki)
- Udongo wa Magadi-Chumvi (Salaini-Sodiki)

### MBINU ZA KUDHIBITI CHUMVI KWENYE UDONGO

- A – Rekebisha udongo ili uondokane na tatizo la chumvi  
B – Tumia mbegu za mpunga au mazao mengine zinazovumilia mazingira ya chumvi au magadi  
C – Changanya mbinu A na B kwa pamoja

Hata hivyo, unashauriwa kutumia mbinu husishi “C”, inayojumuisha urekebishaji wa udongo uondokane nachumvi pamoja na matumizi ya mbegu zinazostahimili chumvi kwa kuwa aina zote za udongo ulioathiriwa na chumvi zaweza kupatikana kwa viwango tofauti kwenye shamba moja.



@Tari tv



@Tari Tanzania



@tari

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:  
Meneja wa Kituo  
TARI Dakawa  
S.L.P 1892, Morogoro, Tanzania  
Simu: (+255) 23 2934300,  
Baruapepe: cmdakawa@tari.go.tz